

FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL11

KISWAHILI PAPER 3 QUESTIONS

1. SEHEMU YA A: USHAIRI (Alama 20)

LAZIMA

1. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

Shairi A

Nimeona, milima na mabonde, misitu na nyika
Nimeona, majani na umande, uliotandazika
Nimeona, mkulima yuwenda shambani

Nimeona, uwanda na magugu, yalomkabili
Nimeona, wajibu na vurugu, wiano mkali
Nimeona, mkulima akiwa tayari

Nimeona, kwa ari na juhudi, anatupa jembe
Nimeona, kakaza ukaidi, kwa nguvu achimbe
Nimeona, mkulima akiwa kazini

Nimeona, kijua kinawaka, kama jahanamu!
Nimeona, jembe lainuka, linapohujumu
Nimeona, mkulima akiwa mbioni.

Nimeona, mvua yamiminika, naye hatohisi
Nimeona, kwa kani anatimika, bila wasiwasi
Nimeona, mkulima akiwa kazini.

Shairi B

Wakati miaka inaibwa mmoja mmoja
Kurudi nyuma, kusimama, kupunguza mwendo
Siwezi kama gurudumu, kupunguza mwendo
Mtelemko mkali huu
Lini na wapi mwisho sijui

Mbele chui mweusi, nyuma mwanga
Nionako kwa huzuni vifurushi maelfu vya dhambi
Kisu, maisha kafiri haya
Kama kutazama nyuma au mbele
Ni kufa moyo mzima!

Sasa kama simba - mtu shauri nimekata
Ya nyuma sana nisijali ya mbele sana niyakabili
Kwa ujasiri na uangalifu nitazunguka
Nikifuata kamba kama ng'ombe aliyefungwa
Kila mpigo wa moyo wangu
Huu mpigo muziki wa maisha
Na sioni, jasho linapomwaika, yendapo mazao
Na sioni, hadhiye kutukuka, ila kilio
Kwa nini? Nauliza mkulima, kwani?

Maswali

- Onyesha tofauti zinazodhihirika katika mashairi haya
 - Kimuundo (alama 5)
 - Kimaudhui (alama 5)
- Eleza tamathali zozote mbili zinazojitokeza katika mashairi haya. (alama 2)
- Andika ubeti wa tatu katika shairi A kwa lugha ya nathari. (alama 3)
- Thibitisha matumizi ya idhini ya mshairi katika tungo hizi (alama 3)
- Tambua toni ya mwandishi katika mashairi, A na B. (alama 2)

2. SEHEMU B: TAMTHILIA (Alama 20)

Timothy Arege: Mstahiki Meya.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel: +254202319748

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

2. “.....Babu zetu hawakupigania uhuru tuje kusaliti juhudi zao....”
 - a) Dondoo hili linaafiki muktadha gani? (alama 4)
 - b) Fafanua usaliti unaorejelewa katika muktadha huu. (alama 16)
3. Jadili migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya “Mstahiki Meya” na utathmini masuhuhisho yanayopendekezwa.

3. SEHEMU YA C: RIWAYA (Alama 20)

4.
 - a) Kwa kurejelea mifano yoyote mitano Onyesha matumizi ya; Kisengere mbele. (alama 12)
 - b) Dhihirisha kuwa dini ni kati ya maudhui ya riwaya ya kidagaa kimemwozea. (alama 8)
5. Vijana wamesawiriwaje katika riwaya ya kidagaa kimemwozea.

4. SEHEMU D: HADITHI FUPI (Alama 20)

Ken. Walibora na S.A Mohammed. Damu Nyeusi na hadithi nyingine

6. **Mke wangu**

“Niliona fedheha kuu kuwa mimi mwana kindakindaki, nimeona kisonoko nisyeweza Kutoka naye mbele za watu; ingawa kwa yeye mwana Hawa kaolewa na mtu anzali Asiyemtakia wenziwe wamjue”

 - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - b) Jadili sifa za anayezungumziwa (alama 6)
 - c) Jadili sifa za anayezungumza. (alama 6)
 - d) Ni mtafaruku gani uliozuka kati ya mzungumzaji na mzungumziwa. (alama 4)

5. SEHEMU YA E (Alama 20)

FASIHI SIMULIZI

7.
 - a) Ni nini maana ya maigizo katika fasihi simulizi. (alama 2)
 - b) Taja sifa zozote nne za maigizo. (alama 10)
 - c) Eleza dhima zozote nne za maigizo. (alama 8)